# ITIFAKI YA MKATABA WA AFRIKA JUU YA HAKI ZA BINADAMU NA WANAWAKE WA AFRIKA

## MKATABA WA MAPUTO



icj International Commission of Jurists
KENYAN SECTION | Since 1959

**Itifaki ya Mkataba wa Afrika juu ya Haki za Binadamu na Wanawake Afrika**
Mkataba Wa Maputo

Kimechapishwa na:
Tume ya kimataifa ya Wanasheria tawi la Kenya
(The Kenyan Section of the International Commission of Jurists) (ICJ Kenya)

Ofisi ya Nne, Laikipia Town Houses, Barabara ya Laikipia, Kileleshwa
S.L.P 59743-00200 | Ofisi ya Nairobi-Kenya
Simu: 020 208 4836/8 | Simu: 0720 491 549
Faksi: 020 387 5982
Barua pepe : info@icj-kenya.org
Tovuti: www.icj-kenya.org
Facebook: https://www.facebook.com/ICJ.Kenya
Twitter: twitter.com/#!/icjkenya

Mchoro na mpangilio wa Fumba la Kitabu umefanywa na:
Silas Kamanza
Afisa wa Kitengo/Programu ya Upatikanaji wa Haki, ICJ Kenya
ngalaakamanza@gmail.com; silas.kamanza@icj-kenya.org

Mpangilio wa maneno umefanywa na:
Brian Ahona
brianahona@gmail.com

Mpiga picha: Mchoro umefanywa na mchoraji asiyejulikana, picha imetolewa kwa tovuti hii: http://www.rebrandafrica.blogspot.co.ke/p/rebranding-con - cept.html, 2016

©2016 Haki za umiliki za kitabu hiki imelindwa na tume ya kimataifa ya Wanasheriatawi la Kenya (ICJ kenya). ICJ Kenya inapeana ruhusa (ya) kuchapisha sehemu ya vitabu vyake bila malipo, kwa sharti kwamba nakala hiyo imetumwa katika afisi zake kupitia anuani ambayo imepeanwa hapo juu.

# Yaliyomo


**Utangulizi** i

**Kifungu cha 1:** Maelezo 1

**Kifungu cha 2:** Kuondoa ubaguzi dhidi ya wanawake 2

**Kifungu cha 3:** Haki ya heshima 4

**Kifungu cha 4:** Haki ya maisha, uadilifu na usalama wa mtu 4

**Kifungu cha 5:** Kuondoa vitendo hatari 6

**Kifungu cha 6:** Ndoa 7

**Kifungu cha 7:** Kutengana, talaka na kubatilisha kwa ndoa 9

**Kifungu cha 8:** Kupata haki na kulindwa sawa kisheria 9

**Kifungu cha 9:** Haki ya Kushiriki katika siasa na Mchakato wa Kufanya Maamuzi 10

**Kifungu cha 10:** Haki ya amani 11

**Kifungu cha 11:** Ulinzi wa Wanawake katika Migogoro ya Silaha 12

**Kifungu cha 12:** Haki ya elimu na mafunzo 13

**Kifungu cha 13:** Haki za kijamii na kiuchumi 14

**Kifungu cha 14:** Afya na haki za afya ya uzazi 16

**Kifungu cha 15:** Haki ya usalama wa chakula 18

**Kifungu cha 16:** Haki ya kuwa na makao bora 18

**Kifungu cha 17:** Haki ya tamaduni nzuri 18

**Kifungu cha 18:** Haki ya kuishi katika mazingira endelevu na yenye afya nzuri 19

**Kifungu cha 19:** Haki ya maendeleo endelevu 20

**Kifungu cha 20:** Haki za wajane 21

**Kifungu cha 21:** Haki ya kurithi 21

**Kifungo cha 22:** Ulinzi maalum kwa wanawake wazee 22

**Kifungu cha 23:** Ulinzi maalum kwa wanawake wanaoishi na ulemavu 22

**Kifungu cha 24:** Ulinzi maalum kwa wanawake walio katika Shida 23

**Kifungu cha 25:** Fidia 23

**Kifungu cha 26:** Utekelezaji na Ufatiliaji 24

**Kifungu cha 27:** Ufasiri 24

**Kifungu cha 28:** Sahihi, uidhinishaji na Utumizi 25

**Kifungu cha 29:** Kuanza Kutumika 25

**Kifungu cha 30:** Marekebisho na Marudio 25

**Kifungu cha 31:** Hali ya Itifaki hii 26

**Kifungu cha 32:** Mipango ya Mpito 27

# Utangulizi

Tume ya Kimataifa ya Wanasheria Tawi la Kenya (The Kenyan Section of the International Commission of Jurists), (Tume ya ICJ Kenya) imekuwa ikifwatilia, kwa kina, utekelezaji wa **Itifaki ya Maputo** kupitia njia tofauti mojawapo ikiwa mafundisho kwa maafisa wa sheria katika nchi za Afrika Mashariki na uzalishaji wa zana za ujuzi kuhusu maudhui ya itifaki hiyo. Madhumuni ikiwa ni kukuza matumizi ya itifaki hii na kuchangia katika stakabadhi zinazoendeleza haki za wanawake katika nchi za Afrika Mashariki. Tume ya ICJ Kenya pia imechapisha kitabu kinachokusanya kesi zilizoamuliwa na Mahakama za Afrika Mashariki kuhusu haki za wanawake kulingana na itifaki ya Maputo. Kitabu hiki kitatumiwa katika mafunzo ya maafisa wa mahakama na wanasheria ili kuhimiza matumizi miongoni mwao.

Ili kuhakikisha utetezi endelevu kwa ajili ya utekelezaji, ICJ Kenya imeunda toleo rahisi la itifaki ya Maputo ambayo ni rahisi kusoma na kuelewa. Toleo hili linalenga watu mbalimbali kama; wamiliki wa haki; maafisa wa mahakama; mawakili wanaotetea haki za wanawake; mashirika ya kiserikali; taasisi za kitaaluma, mashirika ya kiraia, mashirika ya kijamii, na umma kwa ujumla.

ICJ Kenya ina matumaini kwamba toleo hili rahisi la itifaki ya Maputo litatumika kama chombo cha utafiti, utetezi wa haki na kupeleka kesi za haki za wanawake mahakamani. Inatarajiwa kuwa toleo hili

litazidisha umaarufu wa itifaki ya Maputo, na kurahisisha ufahamu wa vipengele vyake.

ICJ Kenya inachukua fursa hii kushukuru baraza lake la uongozi na wafanyikazi wote kwa mchango na jitihada zao za pamoja katika kuhakikisha kuwa toleo hili limetafsiriwa na kuchapishwa vilivyo.

ICJ Kenya inazidisha shukrani zake kwa shirika la American Jewish World Service kwa kufadhili uchapishaji wa kitabu hichi.

Shukrani,



Samwel Mohochi

Mkurugenzi Mkuu

Tume ya kimataifa ya wanasheria-

Tawi la Kenya

**ITIFAKI YA MKATABA WA AFRIKA JUU YA HAKI ZA BINADAMU NA WANAWAKE WA AFRIKA**

**Nchi mwanachama wa itifaki hii,**

**TUKIZINGATIA** kifungu cha sitini na sita cha Mkataba wa Afrika juu ya haki za binadamu inapeana mkataba au makubaliano ya kipekee, ikiwezekana, kuongezea kwa hati za Afrika. Wakikutana katika kikao cha thelathini na moja jijini Addis Ababa, Ethiopia, Mwezi wa Juni mwaka wa 1995, Muungano wa Maraisi na Serikali ya Shirika la Umoja wa Kiafrika walitia sahihi makubaliano AHG/Res.240 (xxxI) ya mapendekezo ya Tume ya Afrika ya Haki za Kibinadamu na watu ili kufafanua zaidi itifaki ya haki za wanawake barani Afrika;

**TUKIZINGATIA** kifungu cha pili cha Mkataba wa Afrika juu ya Haki za binadamu, inajumuisha kanuni ya kutobagua kwa misingi ya rangi, kabila, jinsia, lugha, dini, siasa au maoni mengine yoyote, asili ya kitaifa na jamii, bahati, kuzaliwa au hali nyingine;

**TUKIZINGATIA ZAIDI** kuwa kifungu cha kumi na nane cha mkataba wa Afrika juu ya haki za binadamu inatoa wito kwa nchi mwanachama kuondoa ubaguzi dhidi ya wanawake na kuhakikisha kulindwa kwa haki za wanawake kulingana na maazimio ya kimataifa na makubaliano;

**IJULIKANE** kuwa kifungu cha 60 na 61 cha hati ya Afrika kuhusu haki za binadamu inatambua haki za binadamu za kijumuia na kimataifa na mienendo ya kiafrika zikiambatana na kanuni za kimataifa kuhusu haki za binadamu kama zenye umuhimu kwa matumizi na ufafanuzi wa hati ya Afrika;

**IKUMBUKWE** kuwa haki za wanawake zimetambulika na kukubaliwa katika vyombo vyote vya kimataifa,kama vile Makubaliano ya haki za binadamu ulimwenguni, agano la kimataifa la haki za uraia na kisiasa,agano la kimataifa la uchumi, haki za kijamii na za kitamaduni, makubaliano ya kumaliza aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake na itifaki ya kipekee. Hati ya Afrika kwa haki na ustawi wa mtoto, na makubaliano na maagano ya kimataifa yanayohusiana na haki za wanawake, haki ambazo zinategemeana na haziwezi kutenganishwa;

**IJULIKANE** kuwa haki na mchango wa wanawake unachangia pakubwa katika maendeleo, na imesisitizwa katika mipango ya Umoja wa Mataifa ya Mazingira na Maendeleo (United Nations Plans of Action on the Environment and Development) ya mwaka wa 1992 sawia na haki za binadamu mwaka wa 1993, idadi ya watu na maendeleo mwaka wa 1994 na kwa maendeleo ya jamii mwaka wa 1995;

**NA IKUMBUKWE PIA** katika maazimio ya baraza la Umoja wa Mataifa la usalama 1325 (2000) kuhusu mchango wa wanawake kwa kuendeleza amani na usalama;

**TUKIHAKIKISHA** kanuni ya kuendeleza usawa wa kijinsia kama ulivyothibitishwa katika sheria za umoja wa Afrika na ushirikiano mpya wa maendeleo ya Afrika, maazimio yanayokubalika, maamuzi na makubaliano, ambayo yanaangazia kujitolea kwa mataifa ya Afrika na kuhakikisha kuwa wanawake wanatoa mchango mkubwa katika maswala ya maendeleo Afrika;

**TUKIANGALIA ZAIDI** jukwa la Afrika la vitendo na azimio la Dakar la 1994 na jukwa la Beijing la 1995 linatoa wito kwa wanachama wa nchi za umoja wa mataifa, ambao wamejitolea kuzitekeleza, kuchukua hatua mwafaka na kuzingatia haki za binadamu za wanawake ili kuondoa aina yeyote ya ubaguzi na unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya wanawake;

**IKITAMBULIKA** wajibu wa wanawake kwa kulinda maadili ya kiafrika kulingana na kanuni za usawa, amani, uhuru, heshima, haki, umoja na demokrasia;

**TUKIKUMBUKA** maazimio yanayohusiana, makubaliano, maamuzi, maagano na vyombo vingine vya maeneo na maeneo madogo ambayo yamelengwa kwa kuondoa kila aina ya ubaguzi na kuendeleza usawa baina ya wanawake na wanaume;

**TUKIWA** na wasiwasi kuwa licha ya kuidhinisha Hati ya Afrika kuhusu haki za binadamu sawia na sheria za kimataifa za haki ya binadamu na nchi nyingi ambazo ni wanachama na kujitolea kwao kuondoa kila aina ya ubaguzi na vitendo hatari kwa wanawake, wanawake wengi Afrika wanaendelea kuwa waathiriwa wa ubaguzi na vitendo hatari;

**TUNAAMINI** kuwa kitendo chochote ambacho kinahatarisha kukuwa kwa kawaida na kinaathiri kuendelea kimawazo na kimwili kwa wanawake na wasichana kinafaa kukashifiwa na kuondolewa;

**TUNAJITAHIDI** kuhakikisha kuwa haki za wanawake zimekuzwa, zimejulikana na kulindwa ili kuwawezesha kuzifurahia.

**YAFUATAYO NDIO MAKUBALIANO**

## Kifungu cha 1

### Maelezo

Kwa ajili ya Itifaki hii:

“Mkataba wa Afrika” inamaanisha Mkataba waAfrika juu ya haki za binadamu na watu;

1. “Tume ya Afrika” inamaanisha Tume ya Afrika kuhusu haki za binadamu na watu;
2. “Baraza” Baraza la Maraisi na Serikali ya Muungano wa Afrika;
3. “AU” Inaamanisha muungano wa Afrika;
4. “Sheria ya kujumuisha” inaamanisha sheria ya maadili ya muungano wa Afrika;
5. “Ubaguzi dhidi ya wanawake” inamaanisha kutengwa kwa aina yeyote, kuondolewa au kuzuiliwa au kuangaliwa kwa mtazamo tofauti kwa sababu ya jinsia na ambayo nia au matokea yake yanaharibu kutambulika, kufurahia kwa wanawake, bila kujali hali yao ya ndoa, kwa haki za binadamu na uhuru sawa katika nyanja zote za maisha;
6. “Vitendo hatari” inamaanisha tabia zote, mienendo, mitazamo na vitendo ambavyo vinaathiri haki za wanawake na wasichana kama vile haki yao ya maisha, afya, heshima, elimu na heshima ya kimwili;
7. ‘‘NEPAD” inamaanisha Ushirikiano mpya wa maendeleo ya Afrika ambao uliundwa na Baraza;

8. “Nchi wanachama” inamaanisha nchi ambazo zimekubali itifaki hii;
9. “Unyanyasaji dhidi ya wanawake” inamaanisha vitendo vyote ambavyo vimetekelezwa kwa wanawake ambavyo vinasababisha au vinaweza kusababisha kuumia kimwili, kimawazo, kijinsia na kiuchumi pamoja na tisho la kufanya vitendo hivyo; vizuizi vya kiholela au uhuru wao katika sehemu za kibinafsi au za umma kwa wakati wa amani na wakati wa vita vyenye silaha au mapigano makali;
10. “Wanawake” inamaanisha watu walio na umbo la kike wakiwemo wasichana

## Kifungu cha 2

### Kuondoa ubaguzi dhidi ya wanawake

1. Nchi wanachama zitazuia aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake kupitia njia za kisheria, taasisi na hatua nyengine kulingana na suala hili nchi hizi zitahitajika kufanya;

   a. Weka katika katiba zao za nchi na vyombo vingine vya sheria, kama hazijaweka, kanuni ya usawa kati ya wanawake na wanaume na kuhakikisha imetekelezwa;

b. Tunga na kutekeleza vilivyo sheria au njia za kudhibiti pamoja na kuzuia aina zote za ubaguzi hasa vile vitendo vinavyohatarisha afya na ustawi wa wanawake kwa jumla;
c. Jumuisha sheria za kijinsia katika maamuzi ya sera, kutunga sheria, mipango ya maendeleo, miradi na vitendo katika kila nyanja ya maisha;
d. Chukua hatua ya kurekebisha kisheria sehemu ambazo ubaguzi wa wanawake unaendelea kutumika;
e. Unga mkono mipango ya kitaifa, kimataifa, kikanda na kibara iliyoelekezwa katika kukomesha aina zote za ubaguzi dhidi ya wanawake;
f. Nchi wanachama zitajitolea zenyewe kuimarisha mienendo ya kijamii na ya kitamaduni ya tabia za wanawake na wanaume kupitia elimu ya umma, habari, elimu na mikakati ya mawasiliano, na lengo la kufikia kuzuia vitendo vya mila na tamaduni na vitendo vingine ambavyo vimeegemea kwa kuwa na nguvu au kutokuwa na nguvu kwa jinsia yeyote, au kuendeleza misemo isiyo sawa kuhusu nafasi za wanawake na wanaume.

## Kifungu cha 3

### Haki ya heshima

1. Kila mwanamke atakuwa na haki ya kuheshimiwa ambayo iliyo asili ya kibinadamu na kwa kutambua haki zake za kisheria na za kibinadamu.
2. Kila mwanamke atakuwa na haki ya kuheshimiwa kama binadamu na kuwa huru kujiendeleza kwa maendeleo yake kibinafsi.
3. Nchi wanachama zitapitisha na kutekeleza hatua zinazofaa kuzuia unyanyasaji wowote au ushushaji wa hali ya wanawake.
4. Nchi mwanachama zitapitisha na kutekeleza hatua zinazofaa kuhakikisha ulinzi wa haki ya kila mwanamke, kwa minajili ya kulinda heshima ya wanawake kutokana na aina zozote za vurugu, hasa unyanyasaji wa kijinsia na matusi.

## Kifungu cha 4

### Haki ya maisha, uadilifu na usalama wa mtu

1. Kila mwanamke atahitajika kuheshimiwa katika maisha yake na uadilifu na usalama wake kama binadamu. Kila aina ya unyanyasaji, ukatili, kutokuwa na utu au kushusha hadhi ya mtu itakataliwa kabisa.
2. Nchi wanachama zitazingatia njia mwafaka kwa:

a. Kutunga na kutekeleza sheria ili kuzuia kila aina ya dhuluma dhidi ya wanawake ikiwemo ngono isiyo kubalika na ya kulazimishwa ikiwa imefanyika kisiri au wazi;
b. Kukubali njia nyengine mwafaka za sheria, usimamizi, za kijamii na kiuchumi kusaidia kuzuia, kuadhibu na kumaliza kila aina ya dhuluma dhidi ya wanawake;
c. Kutambua sababu na matokeo ya unyanyasaji dhidi ya wanawake na kuchukua hatua zinazofaa kuzuia na kuondoa dhuluma hizo;
d. Kusaidia Kuendeleza elimu kuhusu amani kupitia mtaala shuleni na kuzungumzia jamii ili kuondoa vipengele vya utamaduni, mila na itikadi, vitendo na uenezaji wa habari isiyo sahihi ambayo inaendeleza na kukubali kuwepo na kuvumilia kwa vita dhidi ya wanawake;
e. Kuadhibu wanaotekeleza dhuluma dhidi ya wanawake na kutekeleza miradi ya kuwapa ushauri wanawake waathiriwa wa vita;
f. Kutunga mbinu za kupokea huduma ambazo zinaweza kufikiwa ili kupata habari muhimu, na kuwarudisha wanawake walioathirika katika hali yao ya kawaida;
g. Kuzuia na kulaani ulanguzi wa wanawake, kuwashtaki watuhumiwa wa ulanguzi wa wanawake na kuwalinda wanawake ambao wako katika hali ya hatari;

h. Kuzuia kila aina ya uchunguzi wa kisayansi kwa wanawake bila idhini yao;
i. Kutenga fedha za kutosha na rasilimali nyengine kwa ajili ya utekelezaji na ufatiliaji wa shughuli zinazolenga kuzuia na kukomesha dhulma dhidi ya wanawake;
j. Kuhakikisha kuwa nchi ambazo hukumu ya kifo bado ingalipo, wasitekeleze hukumu hiyo kwa wanawake wajawazito au wanaonyonyesha;
k. Kuhakikisha kwamba wanawake na wanaume wanapata haki sawa za mapokezi kwa wakimbizi na kwamba wanawake wakimbizi wanapewa ulinzi kikamilifu na wananufaika na sheria za kimataifa zinazolinda wakimbizi ikiwemo stakabadhi za kuwatambua miongoni mwa stakabadhi nyengine hitajika.

## Kifungu cha 5

### Kuondoa vitendo hatari

Nchi wanachama zitakataa na kulaani kila aina ya vitendo hatari vinavyoathiri vibaya haki za kibinadamu za wanawake ambazo haziambatani na viwango vya kimataifa. Nchi wanachama zitachukua hatua za kisheria na hatua nyengine kuondoa vitendo kama hivyo, ikiwemo:

a. Kuhamasisha umma katika vitengo vyote vya jamii kuhusiana na vitendo hatari kupitia habari, elimu rasmi, elimu isiyo rasmi na miradi zingine za kijamii;
b. Kukataa, kupitia njia za kisheria ikiwemo kuwekewa vikwazo, kwa visa vya ukeketaji wa wanawake, kutishia, kutumia njia za udaktari za dharura kwa ajili ya ukeketaji na vitendo vingine ili viweze kukomeshwa;
c. Kutoa misaada muhimu kwa waathiriwa wa vitendo hatari kupitia huduma za kimsingi kama huduma za faya, msaada wa kisheria kihisia na kisaikolojia na pia masomo ya kuwasaidia kujikimu kimaisha ili kuwawezesha kuwa watu wakujitegemea;
d. Kulinda wanawake walio katika hatari ya kutendewa vitendo hatari au aina zingine za vita, dhuluma na usumbufu.

## Kifungu cha 6

### Ndoa

Nchi wanachama zitahakikisha kuwa wanawake na wanaume wanafurahia haki sawa na wanachukuliwa kama wahusika sawa katika ndoa. Na pia watatunga sheria za kitaifa zitakazohakikisha kuwa:

a. Hakuna ndoa ambayo itapitishwa bila kukubaliana kwa wahusika wote;
b. Umri wa chini zaidi wa ndoa kwa wanawake uwe miaka 18;

c. Ndoa kati ya mume na mke mmoja ndio inayohimizwa na haki za wanawake katika ndoa na familia, ikiwemo ndoa ya wanawake wengi itazingatiwa na kulindwa;
d. Kila ndoa itaidhinishwa kwa kuandikwa na kusajiliwa kulingana na sheria za nchi, kwa minajili ya kutambulika kisheria;
e. Mume na mke walio kwenye ndoa watakubaliana kuhusu makazi yao;
f. Mwanamke aliye kwenye ndoa atakuwa na haki ya kubakia na jina lake la kifamilia, na kulitumia apendavyo, pamoja au bila jina la mume wake;
g. Mwanamke atakuwa na haki ya kubakia na uraia wake au kuchukua uraia wa mume wake;
h. Mwanamke na mwanamume watakuwa na haki sawa, ikiambatana na uraia wa watoto wao ila iwapo kuna pingamizi za kisheria za nchi hiyo au kulingana na usalama wa nchi hiyo;
i. Mwanamke na mwanamume watachangia kwa pamoja kwa kulinda na kushughulikia familia, kulinda na kuwaelimisha watoto wao;
j. Akiwa katika ndoa, mwanamke atakuwa na haki ya kupata mali yake na kuitumia vile anavyopenda bila wasiwasi.

## Kifungu cha 7

### Kutengana, talaka na kubatilisha kwa ndoa

Nchi wanachama zitatunga sheria za kuwezesha wanawake na wanaume kupata haki sawa wakati wa kutengana, talaka au kubatilisha ndoa. Katika hali hii, watahakikisha kuwa:

a. Kutengana, talaka au kubatilisha ndoa zinatekelezwa kupitia maamuzi ya koti;
b. Wanawake na wanaume watakuwa na haki sawa za kutaka kutengana, talaka na kubatilisha ndoa;
c. Iwapo mwanaume na mwanamke watatengana, talakiana au kubatilisha ndoa, watakuwa na haki na majukumu sawa kwa watoto wao. Hata hivyo maslahi ya watoto yatapewa umuhimu zaidi;
d. Iwapo kuna kutengana, talaka au kubatilisha ndoa, wanawake na wanaume watakuwa na haki ya kugawanya mali ambayo ilipatikana wakati wa ndoa sawa sawa.

## Kifungu cha 8

### Kupata haki na kulindwa sawa kisheria

Wanawake na wanaume wako sawa mbele ya sheria na watakuwa na haki ya kulindwa sawa na kufaidika kisheria. Nchi wanachama zitachukua njia mwafaka kuhakikisha:

a. Wanawake watapokea huduma za mahakama na za kisheria kwa njia iliyo sawa, ikiwa ni pamoja na msaada wa kisheria;
b. Kuunga mkono miradi ya kimaeneo, kitaifa, kikanda na bara iliyoelekezwa kuwapa wanawake huduma za kisheria, ikiwa ni pamoja na msaada wa kisheria;
c. Kuweka miundo sahihi ya kielimu na miradi zingine zitakazozingatia sana wanawake na kuhamasisha kila mmoja kuhusu haki za wanawake;
d. Kuwa viungo vya utekelezaji wa sheria katika nyanja zote vimewezeshwa kufafanua zaidi na kuendeleza haki za kijinsia kwa usawa;
e. Kuwa wanawake wamepata uwakilishaji sawa katika mahakama na vitengo vingine vya sheria;
f. Kurekebisha sheria za ubaguzi zilizopo ili kukuza na kulinda haki za wanawake.

## Kifungu cha 9

### Haki ya Kushiriki katika siasa na Mchakato wa Kufanya Maamuzi

1. Nchi wanachama zitachukua hatua mwafaka za kuendeleza uongozi bora na kuhakikisha kuwa kuna usawa kwa wanawake kushiriki katika siasa nchini mwao na kutambua wanawake kama viongozi wanaofaa, sawia na kuwezesha sheria za nchi kuwa:
    a. Wanawake wanashiriki bila kubaguliwa katika uchaguzi;

b. Wanawake wanapata nafasi sawa za uwakilishi katika ngazi zote za uchaguzi kama wanaume;
c. Wanawake ni washiriki sawa na wanaume katika ngazi zote za maendeleo na utekelezaji wa sera za nchi na miradi ya maendeleo.

2. Nchi wanachama zitazingatia ongezeko na uwakilishi sawa wa wanawake katika ngazi zote za maamuzi.

## Kifungu cha 10

### Haki ya Amani

1. Wanawake wana haki ya kuishi kwa amani na haki ya kushiriki katika shughuli za kuendeleza na kulinda amani.
2. Nchi wanachama zitachukua hatua mwafaka ili kuhakikisha kwamba wanawake wengi wanashiriki:
   a. Katika miradi ya elimu kuhusu amani na tamaduni za amani;
   b. Katika shughuli za mipango ya kuzuia, kuangazia na kutatua vita katika maeneo ya mashinani, kitaifa, kikanda bara na ngazi za kimataifa;
   c. Katika shughuli za maamuzi mashinani, kitaifa, kikanda, kimataifa na kufanya mikakati ya kuhakikisha kuwa wakimbizi, wanaotafuta hifadhi, waliorudi makwao na wale wakimbizi wa ndani kwa ndani hasa wanawake

wanapata ulinzi wa kimazingira, kisaikolojia, kijamii na kisheria.

d. Katika ngazi zote za usimamizi wa kambi za wakimbizi, wanaotafuta hifadhi, waliorudi kutoka makwao na wakimbizi wa ndani kwa ndani hasa wanawake.

e. Katika mipangilio yote ya kuunda na kutekeleza shughuli za kuwarekebisha na kuwarudisha katika hali yao ya kawaida.

3. Nchi wanachama zitachukua hatua mwafaka za kupunguza utumizi wa fedha kwa jeshi ili fedha hizo zitumike kwa shughuli za kijamii na maendeleo kwa jumla hasa kwa wanawake.

## Kifungu cha 11

### Ulinzi wa Wanawake katika vita vya Silaha

1. Nchi wanachama zitazingatia na kuheshimu sheria ya kimataifa ya kibinadamu inayohusika katika migogoro yenye silaha, ambayo huathiri idadi ya watu, hasa wanawake.
2. Nchi wanachama zitafanya kazi kulingana na matakwa ya sheria za kimataifa za binadamu, kulinda raia pamoja na wanawake, pasipo kujali idadi ya watu ambako wametoka, wakati wa vita vya silaha.
3. Nchi wanachama zitawalinda wanawake wanaotoroka vita, wakimbizi, wanaorudi kutafuta makao na wakimbizi wa ndani kwa ndani, dhidi ya aina yeyote ya vita, unajisi na njia nyengine

za unyanyasaji wa kijinsia, na kuhakikisha kuwa vitendo kama hivyo vinatambulika kama makosa ya kivita, mauwaji ya kikabila au makosa dhidi ya binadamu na kuwa waliotenda makosa wanashtakiwa katika mahakama ambayo inatambulika.

4. Nchi wanachama zitachukua hatua zinazofaa kuhakikisha kuwa kila mtoto, hasa wasichana walio chini ya miaka kumi na nane, wasihusike katika njia yeyote ile katika vita na kuwa mtoto yeyoto asisajiliwe kama jeshi wa kupigana vita.

## Kifungu cha 12

### Haki ya elimu na mafunzo

1. Nchi wanachama zitachukua hatua mwafaka:
    a. Kuondoa kila aina ya ubaguzi dhidi ya wanawake na kuhakikisha nafasi sawa za kupokea elimu na mafunzo;
    b. Kuondoa kila aina ya ubaguzi katika vitabu, mtaala wa masomo, na katika vyombo vya habari, ambao utaendeleza tabia za kubaguliwa;
    c. Kulinda wanawake, hasa mtoto wa kike kutokana na kila aina ya dhulma, ikiwemo kunyanyaswa kimapenzi katika shule na taasisi nyengine za elimu na kupeana vikwazo kwa idhini ya kushikwa kwa wanaoendeleza vitendo hivyo;
    d. Kupeana huduma za ushauri na kuwarekebisha wanawake ambao wamedhulumiwa na kunyanyaswa kimapenzi;

   e. Kujumlisha mafundisho ya kijinsia na haki za kibinadamu katika ngazi zote za elimu ikiwemo taasisi za mafunzo ya walimu.

2. Nchi wanachama zitazingatia mipango maalum:
   a. Kuendeleza masomo miongoni mwa wanawake;
   b. Kuendeleza elimu na mafundisho kwa wanawake katika ngazi zote na nyanja zote za maisha, hasa katika taaluma za sayansi na teknolojia;
   c. Kuendeleza kusajiliwa kwa wasichana shuleni na katika taasisi nyengine za elimu na kuwafanyia miradi wasichana wanaowacha masomo mapema.

## Kifungu cha 13

### Haki za kijamii na kiuchumi

Nchi wanachama zitazingatia na kutekeleza sheria na mipango zingine za kuwapa wanawake nafasi sawa katika kazi zao na kuendeleza taaluma zao na nafasi zingine za kiuchumi. Katika hali hii, wata:

a. Endeleza usawa katika nafasi za ajira;
b. Endeleza haki ya kupokea mshahara sawa katika kazi ambazo wanawake na wanaume wanafanya kwa pamoja;

c. Hakikisha uwazi katika kupeana nafasi za ajira, kupandishwa cheo na kuwachishwa kazi kwa wanawake, kuzuia na kuadhibu vitendo vya dhuluma za kimapenzi kazini;
d. Hakikishia wanawake uhuru wa kuchagua kazi wanayopenda, na kuwalinda dhidi ya kudhulumiwa na waajiri wao ambao wanakiuka na kuwanyima haki zao za kimsingi zinazotambulika na kuzingatiwa katika makubaliano, sheria na taratibu zilizoko;
e. Unda mazingira ya kuendeleza na kusaidia kazi na shughuli za kiuchumi kwa wanawake, hasa katika sekta ya jua kali;
f. Unda mfumo wa bima ya kijamii ya kulinda wanawake ambao wanafanya kazi katika sekta za jua kali na kuwaelimisha kuhusu umuhimu wa kufuata mfumo huo;
g. Toa kiwango cha chini cha miaka ya kufanya kazi na kukataa kuajiriwa kwa watoto chini ya miaka hiyo, kukataa, na kuadhibu kila aina ya unyanyasaji wa watoto, hasa mtoto wa kike;
h. Zingatia na kutambua hatua mwafaka za kiuchumi ambazo wanawake wanafanya nyumbani;
i. Hakikisha kuna likizo na malipo kabla na baada ya likizo ya wanawake wanapojifungua katika sekta za kibinafsi na za umma;
j. Hakikisha utozwaji sawa wa ushuru kwa wanawake na wanaume;

k. Tambua na kutekeleza haki ya wanawake kupokea mshahara na marupurupu na manufaa mengine kama vile wanaume ambao wana wake na watoto wanavyopewa;
l. Tambua kwamba wazazi wote wako na majukumu ya kulea watoto na kwamba ni shughuli ya kijamii ambayo nchi na sekta za kibinafsi ziko na majukumu ya ziada;
m. Chukua njia mwafaka za kisheria na usimamizi ili kuzuia kunyanyaswa na kudhulumiwa kwa wanawake dhidi ya matangazo na picha za ngono.

## Kifungu cha 14

### Afya na haki za afya ya uzazi

1. Nchi wanachama zitahakikisha kwamba kuna haki ya kupata huduma za afya kwa wanawake, ikiwemo afya ya uzazi na kimapenzi na kuhakikisha kuwa imeheshimiwa na kuendelezwa. Hii inajumlisha:
    a. Haki ya kuamua kuhusu hali yao ya uzazi;
    b. Haki ya kuamua iwapo watakuwa na watoto, idadi ya watoto na nafasi katikati ya watoto;
    c. Haki ya kuchagua mbinu yoyote ya upangaji uzazi;
    d. Haki ya kujikinga na kulindwa kutokana na magonjwa ya ziinaa ikiwemo ugonjwa wa ukimwi;

e. Haki ya kujulishwa kuhusu hali yako ya kiafya na hali ya afya ya mpenzi wako, haswa iwapo ameathirika na ugonjwa wa zinaa ikiwemo ugonjwa wa ukimwi, kulingana na kanuni bora za kimataifa;
f. Haki ya kupokea elimu ya mbinu za upangaji uzazi.

2. Nchi wanachama zitazingatia hatua zifuatazo
    a. Kupeana huduma bora za afya ambazo watu wanaweza kulipia ikiwemo habari; elimu na miradi ya mawasiliano hasa kwa wanawake wanaoishi mashambani;
    b. Kuanzisha na kutilia mkazo afya ya mama kabla na baada ya kujifungua na huduma kuhusu lishe bora kwa wanawake wajawazito na wanaonyonyesha;
    c. Kulinda haki za afya ya uzazi kwa wanawake kwa kuidhinisha uavyaji mimba iwapo wamenyanyaswa kimapenzi, kunajisiwa, kufanya mapenzi na mtu wa ukoo, na iwapo mimba hiyo inahatarisha akili au afya ya kimwili ya mama au mtoto aliye tumboni.

## Kifungu cha 15

### Haki ya usalama wa chakula

Nchi wanachama zitahakikisha kuwa wanawake wana haki ya kupata chakula chenye virutubisho muhimu. Katika hali hii, watahakikisha kuwa:

a. Wanawake wanapata maji safi ya kunywa, vyanzo vya mbinu asilia vya kutumia kupika, shamba, na njia za kukuza vyakula ambavyo vina virutubisho muhimu;
b. Wanaanzisha mbinu za kusambaza na kuweka chakula ili kuwe na usalama wa chakula.

## Kifungu cha 16

### Haki ya kuwa na makao bora

Wanawake watakuwa na haki ya kupata makao na mazingira bora na yanayokubalika. Ili kuhakikisha haki hii inazingatiwa, nchi wanachama zitawapa kina mama, chochote wanachohitaji bila kuangalia hali yao ya ndoa, ili kupata makao bora ya kuishi.

## Kifungu cha 17

### Haki ya tamaduni nzuri

1. Wanawake watakuwa na haki ya kuishi katika hali ya tamaduni nzuri na kuchangia katika ngazi zote na kutambua sera za tamaduni hizo.

2. Nchi wanachama zitazingatia njia za kuendeleza ushiriki wa wanawake katika uundaji wa sera za utamaduni wao katika ngazi zote.

## Kifungu cha 18

### Haki ya kuishi katika mazingira endelevu na yenye afya nzuri

Wanawake watakuwa na haki ya kuishi katika mazingira bora na yenye afya endelevu.

Nchi wanachama zitazingatia njia hizi ku:

a. Hakikisha wanawake wanashirikishwa pakubwa katika mipango, usimamizi, kulinda mazingira na utumiaji mzuri wa rasilimali katika ngazi zote;

b. Saidia kuendeleza utafiti na uwekezaji katika kupata nishati mbadala inayotokana kwa njia za kiasili na mbinu za kisasa zinazokubalika, ikiwemo mbinu za teknolojia ya kisasa na kuwawezesha wanawake kujisimamia katika hali hiyo;

c. Linda na kuwezesha kuendelea kwa mifumo ya kiasilia kwa wanawake;

d. Simamia, kutengeneza, kuweka na kutupa uchafu wa nyumbani;

e. Hakikisha kuwa viwango vinavyofaa katika kuweka, kusafirisha na kutupa uchafu ambao ni hatari vimezingatiwa.

## Kifungu cha 19

### Haki ya maendeleo endelevu

Wanawake watakuwa na haki ya kunufaika kutokana na haki ya maendeleo endelevu. Na katika hali hii, nchi wanachama zitazingatia njia mwafaka ku:

a. Anzisha mtazamo wa kijinsia katika mipangilio ya maendeleo ya kitaifa;

b. Hakikisha wanawake wanashirikishwa katika ngazi zote za maamuzi, utekelezaji na tathmini ya sera na miradi ya maendeleo;

c. Endeleza uwezo wa wanawake kupata na kudhibiti rasilimali kama vile ardhi na kuwahakikishia haki yao ya kumiliki mali;

d. Endeleza upatikanaji wa mikopo kwa wanawake, mafunzo na ujuzi wa maendeleo na huduma katika ngazi za mashambani na mijini ili kuwawezesha wanawake kupata maisha bora na kupunguza viwango vya umasikini miongoni mwao;

e. Tilia maanani viashiria vya maendeleo ya kibinadamu hasa vinavyohusiana na wanawake kwa kufafanua sera za maendeleo na miradi; na

f. Hakikisha kwamba madhara mabaya ya utandawazi yanayotokana na utekelezaji wa sera za kibiashara na kiuchumi yanapunguzwa kwa minajili ya wanawake.

## Kifungu cha 20

### Haki za wajane

Nchi wanachama zitachukua hatua za kisheria zinazofaa ili kuhakikisha kuwa wajane wanafurahia haki zote za kibinadamu kupitia utekelezaji wa masharti yafuatayo:

a. Wajane wasitendewe vitendo vya kinyama, vya kufedhehesha ama vya kuwashusha hadhi;
b. Mjane atakuwa mlezi wa watoto wake bila kupingwa, baada ya kifo cha mume wake, isipokuwa kama itakuwa ni kinyume na mapenzi na ustawi wa watoto;
c. Mjane atakuwa na haki ya kuolewa tena, na katika hali hiyo, aolewe na mume ambaye ni chaguo lake.

## Kifungu cha 21

### Haki ya kurithi

1. Mjane atakuwa na haki sawa ya kurithi mali ya mume wake. Mjane atakuwa na haki ya kuendelea kuishi katika nyumba yake ya ndoa. Endapo ataolewa tena, atahifadhi haki ya umiliki kama nyumba ni yake ama ameirithi.
2. Wanawake na wanaume watakuwa na haki sawa ya kurithi, mali ya wazazi wao.

## Kifungo cha 22

### Ulinzi maalum kwa wanawake wazee

Nchi wanachama zitakubali ku:

a. Peana ulinzi kwa wanawake wazee na kuchukua hatua mwafaka ambazo zinaambatana na hali yao ya kimwili, kiuchumi na mahitaji ya kijamii pamoja na kupata ajira na masomo ya kujiendeleza;
b. Hakikisha wanawake wazee wamepata haki ya uhuru kutokana na dhuluma dhidi yao, ikiwemo dhuluma za kimapenzi, kubaguliwa kulingana na umri wao na haki ya kutunzwa kwa heshima.

## Kifungu cha 23

### Ulinzi maalum kwa wanawake wanaoishi na ulemavu

Nchi wanachama zitakubali ku:

a. Hakikisha wanawake wanaoishi na ulemavu wamelindwa na kutilia maanani mikakati inayohusiana na maumbile yao, kiuchumi na mahitaji yao ya kijamii, ili kuwawezesha kupata;
b. Ajira, kazi ya kulipwa na masomo ya kiufundi pamoja na kushiriki katika shuguli za maamuzi;
c. Hakikisha wanawake wanaoishi na ulemavu wanapata haki ya kuwa huru dhidi ya dhuluma, ikiwemo dhuluma za kimapenzi,

kubaguliwa kwa sababu ya ulemavu wao na haki ya kutunzwa kwa heshima.

## Kifungu cha 24

### Ulinzi maalum kwa wanawake walio katika Shida

Nchi wanachama zitakubali ku:

a. Hakikisha kulindwa kwa wanawake maskini na wanawake wanaosimamia familia ikiwemo vikundi vya wanawake wanaotoka maeneo yaliyotengwa na kuweka mazingira yanayofaa kulingana na hali yao na hali halisi ya kimaumbile, kiuchumi na mahitaji ya kijamii;
b. Hakikisha haki za wanawake wajawazito au wanaonyonyesha au wanaozuiliwa kwa kuwapa mazingira ambayo yanafaa kulingana na haki ya kutunzwa kwa heshima.

## Kifungu cha 25

### Fidia

Nchi wanachama zitazingatia ku:

a. Lipa fidia zinazofaa kwa mwanamke yeyote ambaye haki zake za uhuru, kama zinavyotambulika zimekiukwa;

b. Hakikisha fidia hizo zimeidhinishwa na mahakama yenye uwezo, utawala ama mamlaka ya kisheria ama mamlaka yoyote iliyo na uwezo wa kisheria.

## Kifungu cha 26

### Utekelezaji na Ufatiliaji

1. Nchi wanachama zitahakikisha utekelezaji wa mkataba huu katika ngazi zote za kitaifa na kutoa taarifa kulingana na kifungu cha 62 cha hati ya Afrika, na kuonyesha njia zingine na zakisheria ambazo zimetumika kutambua haki zilizomo katika itifaki hii.
2. Nchi wanachama zitajitolea kutumia njia zote mwafaka hasa kutenga fedha na rasilimali zingine kwa utekelezaji wa haki zilizomo katika itifaki hii.

## Kifungu cha 27

### Ufasiri

Mahakama ya Afrika ya haki za binadamu itachukua jukumu la kutoa maelezo zaidi ambayo yanatokana na matumizi au utekelezaji wa itifaki hii.

## Kifungu cha 28

### Sahihi, Uidhinishaji na Utumizi

1. Itifaki hii itakuwa wazi kwa ajili ya kutia sahihi, kuidhinishwa na kutumika na nchi wanachama kwa mujibu wa taratibu za katibaya nchi zao.
2. Vipengele vya kuidhinishwa au kutumiwa vitawekwa na mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika (AU).

## Kifungu cha 29

### Mwanzo wa Matumizi wa Mkataba wa Maputo

1. Mkataba huu utaanza kutumiwa siku 30 (thelathini) baada ya kuweka sheria ya idhinisho ya 15 (kumi na tano) cha idhinisho.
2. Kwa kila nchi ambayo itakubali mkataba huu baada ya kupitishwa, utaanza kutumika baada ya kuwekwa kwa sheria ya kukubali mkataba huu.
3. Mwenyekiti wa Tume ya Umoja wa Afrika ataeleza wanachama husika kuhusu mwanzo wa matumizi wa mkataba huu.

## Kifungu cha 30

### Marekebisho na Marudio

Kila nchi mwanachama inaweza kuwasilisha ombi kuhusu marekebisho na kuangaliwa upya kwa itifika hii.

1. Ombi la marudio na marekebisho litawasilishwa, kwa maandishi kwa mwenyekiti wa Tume ya Muungano wa Afrika ambaye atawasilisha ombi hilo kwa nchi zote wanachama katika siku thelathini baada ya kupokea ombi hilo.
2. Bunge la muungano, baada ya ushauri kutoka kwa Tume ya Afrika, litachunguza ombi hilo kwa muda wa mwaka mmoja kufuatia idhini ya nchi husika, kulingana na aya ya pili ya kifungu hiki.
3. Marekebisho au marudio hayo yanapaswa kukubaliwa na wengi wa wanachama wa baraza hilo.
4. Marekebisho hayo yataanza kutumika kwa kila nchi mwanachama, ambayo imekubaliana nayo katika siku thelathini (30) baada ya mwenyekiti wa Tume ya Muungano wa Afrika kupokea taarifa ya kukubalika kwa marekebisho hayo.

## Kifungu cha 31

### Hali ya Itifaki Hii: Uhusiano wa Matumizi ya Itifaki hii na Sheria za Nchi Wanachama

Hakuna moja wapo ya matumizi ya itifaki hii itaathiri matumizi mengine zaidi yanayotambua haki za wanawake ambazo zinazopatikana katika sheria za nchi husika au katika maeneo ya mikoa, bara au kimataifa, mikataba au makubaliano ambayo yanatumika katika nchi wanachama.

## Kifungu cha 32

### Mipango ya Mpito

Huku ikisuburiwa kuanzishwa kwa mahakama ya Afrika kuhusu haki za binadamu, Tume ya Afrika ya haki za binadamu itapewa jukumu la kufafanua zaidi utumizi na utekelezaji wa itifaki hii.

Imekubaliwa na kikao cha kawaida cha pili cha mkutano wa baraza la muungano.

Maputo, 11 Julai 2003

KENYAN SECTION | Since 1959

Tume ya kimataifa ya Wanasheria  - Tawi la Kenya
(The Kenyan Section of the International Commission of Jurists) (ICJ Kenya)
Ofisi ya Nne, Laikipia Town Houses,
Barabara ya  Laikipia, Kileleshwa
S.L.P 59743-00200 | Ofisi ya Nairobi-Kenya
Simu: 020 208 4836/8 | Simu 2: 0720 491 549
Faksi: 020 387 5982
Barua pepe : info@icj-kenya.org
Tovuti: www.icj-kenya.org
Facebook: https://www.facebook.com/ICJ.Kenya
Twitter: twitter.com/#!/icjkenya